

MJADALA JUU YA LUGHA

 Somo juu ya—juu ya huku kunena kwa lugha, ni hoja, mnaona, kwa Wapentekoste, nami nimekuwa na m—mjadala mkubwa. Si—sitoi hoja zozote jukwaani, kwa sababu sasa nina—ninadhaminiwa na makundi mbalimbali, na kama—kama mwungwana Mkristo, hakika nisingetaka kumwudhi mtu yeyote. Mimi...Kama wao ni Wakristo vya kutosha kunikaribisha kwao, huku watu wao wameketi hapo, ni—ninataka kuwa ndugu vya kutosha kutosema lolote kulihusu, mnaona. Basi ninahubiri tu ubatizo wa Roho Mtakatifu, na—na halafu wakati wao, wakati...Acheni wafanye watakalo huko.

² Sasa, ninaamini ya kwamba watu waliojazwa na Roho, mnaona, wakati mwingine wanajazwa sana na Roho Mtakatifu hata hawana mamlaka yo—yoyote juu ya lugha yao wenyewe, Ni—ninaamini hilo, *wakati mwingine* hutendeka. Loo, limetendeka kwangu, na limetendeka kwa wengine, na, lakini, mnaona, jambo ni kwamba, Roho Mtakatifu kwanza hana budi kuwa *mle* ndani. Mnaona ninalomaanisha? Hana budi kuwa *mle* ndani kwanza. Mnaona?

³ Ni kama tu iwapo...Kunena kwa lugha ni karama *ya* Roho Mtakatifu. Sasa, kama nilikuwa m—mvulana, nami nilikuwa katika—katika ninii yangu, chini ya mafunzo wa baba na mama yangu, nawe ulitaka kuniasili niwe mwanao, nami nikakupa kisu changu, sasa, una zawadi yangu lakini si mimi. Unaona? Sasa, lugha ni karama *ya* Roho Mtakatifu, hakuna Maandiko katika Biblia yanayosema *ndiyo* Roho Mtakatifu, ni karama *ya* Roho Mtakatifu.

⁴ Sasa angalieni, Matendo 2:38, “Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa *cha* Roho Mtakatifu.” Kwa sababu walikuwa wakistaajabu, kwa sababu “tulimsikia kila mtu akinena kwa lugha yake mwenyewe aliyozaliwa nayo.” Mnaona? Naye alisema kama mkitubu, mtapokea kipawa hicho *cha* Roho Mtakatifu. Sasa, zawadi *ya* William Branham siyo William Branham. Mnaona?

Sasa, kama mtaangalia, mnasema, “Vema, karama ya Mungu ni Roho Mtakatifu.”

Roho Mtakatifu *ni* Mungu, mnaona, kwa hiyo usingeweza—usingeweza kulitumia hapo.

⁵ Vema, kwa kila kitu ninachozungumzia, hakina budi kupatana na Maandiko, Si—sitalipokea. Sasa, ninapokea tu, wakati Yeye anaponiambia, basi Yeye siku zote analiweka wazi kwa Maandiko. Kama hakufanya hivyo, nisingeliliamini, ingawa kadiri Yeye alivyoniambia njiani, hata hivyo kama Yeye aliwahi

kuniambia jambo lolote ambalo si la Kimaandiko, isingekuwa sawa, maana Maandiko ndiyo msingi wetu kabisa. Hatuwezi kuweka—kuweka msingi wo—wokovu wetu juu ya mihemko, ama matukio ya wengine, au juu ya matukio yetu wenyewe, haina budi kuwa ni Neno la Mungu, mnaona, maana hiyo ndiyo—hiyo ndiyo alama ya kweli.

⁶ Sasa, na wakati nilipoanza kwa mara ya kwanza katika mjadala huu ambao Ndugu Leo ana hamu ya kuunasa hapa kwenye kanda, nadhani, ninakiona kikimulikamulika, nadhani kinanasa sasa, nisingekutaka wewe, Ndugu Leo, kutumia hii kudhuru, ama chochote kile, lakini kuninii tu, najua usingefanya hivyo, wala nisingewaambia, ndugu.

⁷ Kama mtu akinena kwa lugha, vema, asiponena kwa lugha hiyo bado si ishara yeye hana. Na kama yeye... Nimewaona watu wakinena kwa lugha kama kumwaga njegere kwenye ngozi kavu ya ng'ombe, haraka tu walivyoweza kwenda, na kuishi na mke wa mtu mwingine. Mnaona? Nimewaona wachawi wakinywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita ibilisi, na kunena kwa lugha. Nimewaona wachawi, na wana-mazingaombwe wa Kihindi, wakati dansi ya fahali inapoingia, nao wangeketi kwenye duara hili kubwa, nao wangetoka na kufanya uchawi wao wote, ndipo daktari wa kiibilisi anaingia, nao wanazunguka-zunguka, na kufanya huku kurukaruka juu chini, wakipiga mayowe, na kupiga-piga hizi ngoma, na—na ndipo mchawi angeingia na kunena kwa lugha na kuwafasiria. Mnaona? Nami nimekuwa katika kambi za wachawi ambako nilitembea humo mwenyewe, na ni ninii sana... ninyi... Ni...

⁸ Hii si kuwashauri mwende kwa mmoja, lakini kama mhudumu, lazima nijue kile ninachozungumzia, sio kuchukua neno la mtu mwingine, kwa sababu ni... la—lazima nijue kibinafsi, mimi mwenyewe. Mnaona? Kwa sababu siwezi kusema Ndugu Jones alisema *hivi*, ama nilisoma *hili* katika kitabu, sina budi kujua kile ninachozungumzia, kwa sababu kuna watu wengi sana wanaonisikiliza, wala hakika sitaki kushuka kwenye siku hiyo ya mwisho pamoja na kundi la watu waliopotea. Lazima nijue, kabisa, kabla sijasema lolote kuhusu hilo kuwa ni kweli.

⁹ Nami nafikiri kila mhudumu anawajibikia hilo kwa kusanyiko lake, watu anaowahubiria somo lolote, anapaswa kuwa na hakika ya kwamba anajua anachozungumzia kabla hajasema lolote.

¹⁰ Na kwa hiyo, nimekuwa kwenye kambi ambamo washirikina, na ambamo piano inashushwa, yenye uzito wa nusu tani, inainuliwa kutoka sakafuni, nalo gita lililo chumbani linakuja likicheza, muziki na kila kitu namna hiyo, nalo koti lililotundikwa ukutani likapita na kuketi kitini kando yako,

visu na uma vikipita, na kuviona, huyo mchawi anaweka— anaweka kipande cha karatasi chini, anachukua penseli na kuilaza juu yake, na kuona roho hii ikija na kukimbia kwenye bomba la stovu na kurudi chini ikicheza *Nyoa Na Kukata Nywele, Maradufu*, kisha inaandika katika lugha zisizojulikana, halafu kijumbe huyu anajinyoosha, anajivuta pamoja namna *hiyo*, na kufasiri hizi, juu na chini namna *hiyo*, na kuelezea, na—na kufasiri lugha hizo, na kusema yale yaliyosemwa. Kwa hiyo huwezi kusema kwamba kunena kwa lugha unaye Roho Mtakatifu, unaona, maana ni—ninajua vizuri zaidi ya hayo.

¹¹ Sasa, kama mtaangalia, hebu tulitumie kwa busara, mnaona, ili mpate kuelewa, na hivyo ndivyo ninavyotaka kufanya jambo hili kwa sababu ninatambua ninazungumza na watu wenye akili, kwa hiyo katika Maandiko, Wakorintho wa Kwanza 12, ilisema kulikuwa... kuna karama tisa za kiroho. Vema basi, lugha zilikuwa moja ya karama hizo *katika* Mwili wa Kristo.

¹² Aisee, hebu tuonyeshe tu, kwa mfano, na kulirahisisha, najua mnalipata, lakini hebu na tuhakikishe kwamba mnalipata. Chumba hiki—hiki ni Mwili wa Kristo, na kwa Roho mmoja sote tunabatizwa kuwa katika chumba hiki. Basi katika chumba hiki kuna kipawa cha kiti cha kustarehe, kuna kipawa cha nuru, kuna kipawa cha kudhibiti joto, kuna kipawa cha kiti cha bembea, kuna kipawa cha sebule, kipawa cha zulia, kuna kipawa cha picha. Mnaona ninalomaanisha? Hivyo ni vipawa, lakini unaingiaje katika Mwili huo? “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja,” ndipo tuna haki ya chochote cha vipawa hivi. Mnaona?

¹³ Kwa hiyo kama kunena kwa lugha, basi, ni ushahidi wa Roho Mtakatifu, vitu hivi vingine vyote havina budi kuwa ni ushahidi wa Roho Mtakatifu, pia, ingekubidi kufanya mambo haya mengine yote, haya mengine: kutabiri, kufasiri, kuwa na hekima, maarifa. Lakini basi Paulo anaendelea kurekebisha hilo, mnaona, kasema, “Je, wote hunena kwa lugha?” La. “Je, wote wana karama ya kufasiri? Lakini Mungu ameweka Kanisani kama apendavyo...” Mnaona? Aliliweka tu namna hiyo.

¹⁴ Halafu kwenye mlango wa 12...Sasa, kama mtarejea mahali nilipoanzisha mjadala wangu, kuchukua ninii yangu... ushahidi wa kwanza wa Roho Mtakatifu, niliuchukua kuwa ni upendo, na hao watu wengine wakachukua kunena kwa lugha, mnaona, kuwa na lugha kama ushahidi.

¹⁵ Sasa, Paulo alisema katika Wakorintho wa Kwanza 13, unaofuata, yeye alisema, sasa, ya kwamba, “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika,” hiyo ni kusema aina zote mbili, “na sina upendo, si kitu mimi. Nijapokuwa na hekima,” sasa, yeye ananena kuhusu karama hizi hapa juu katika ule Mwili, mnaona, mnaona, kuwa na karama hizi bila

Mpaji, mnaona, upendo, mnaona, “nijapokuwa na hekima, na kufahamu maarifa yote ya Mungu,” Maandiko yote, naweza kuziweka pamoja kama mwanatheolojia yeyote mashuhuri, “wala nisiwe na upendo,” ambao ni Roho Mtakatifu, “si kitu mimi.”

¹⁶ Sasa, tunajua ya kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu, hatuna budi kukubali hilo, mnaona, Huyu ni Mungu. Vema basi, Mungu ni upendo. Mnaona? Kwa hiyo mnaweza kuwa na yoyote ya karama za Mungu, bila kuwa na Mungu, Mungu ni upendo. Naye Shetani anaweza kuiga yoyote ya karama hizo. Mnaona? Mnaona, anaweza kuiga karibu chochote, maana yeye hupotosha; dhambi ni haki iliyopotoshwa.

¹⁷ Kwa hiyo katika ule mjadala, yule ndugu mwenye neema, yeye, yeye akiwa ndiye mgeni, nilisema, “Sasa, niko tayari kujadili hili pamoja nawe kama utadumu na Maandiko kabisa, wala usiyaache Maandiko,” kisha nikasema, “basi mwisho wa mjadala kwamba unaweza kunipa mkono, nasi tungali tutajisikia ni ndugu, maana kama sivyo, nisingefanya hivyo, mnaona, maana,” nikasema, “kwa sababu, labda, huo utakapokwisha utajisikia vile vile unavyojisikia, nami vivyo hivyo, pia.

¹⁸ “Lakini kwa kuwa tuna wasimamizi hapa ambao wameapishwa, wafanyabiashara, mwajua, na kadhalika, kwamba wameninii tu—wameninii tu, hawavutiwi na upande wowote, wanachukua tu ukweli wa mambo. Haidhuru uamuzi wao ni nini, ni watu watano ama sita tu, kwenye Maandiko fulani tu, wakati Andiko hili linapotolewa, ni nani anayelichukua? Ni nani hasa aliyetupa nuru juu yake? Huyu ndiye anayesema, unaona.”

¹⁹ Kwa hiyo akaanza kama kawaida Matendo 2:4, mwajua, kwamba “Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha, kama Roho alivyowajalia kunena.” Vema, mimi. . . Kisha akatoka hapo akaenda kwenye—kwenye—kwenye Matendo 10:49, ambapo, “Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia wale walioyasikia hayo maneno.” Vema basi, kisha akaenda kwenye Matendo 19:5, “Paulo akaweka mkono wake juu yao, na Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakanena kwa lugha.”

²⁰ Kwa hiyo hilo lilichukua karibu wakati wake wote, ndipo ikawa ni wakati wangu. Tulikuwa kuanzia saa moja hadi saa nane usiku, mnaona, kwa hiyo ulikuwa ni mrefu. Kwa hiyo basi wakati aliporudi, alikuwa na yapata dakika thelathini ama thelathini na tano juu ya hilo, ndipo wakawapumzisha watu, kisha wakaniruhusu nizungumze tena, wakaniruhusu nizungumze. Kwa hiyo, sikuyaacha Maandiko yake, nilidumu moja kwa moja na Maandiko yake. Hiyo ndiyo njia pekee

unayoweza kwa usahihi, kwa busara...Niko radhi tu kujua ukweli kama mtu mwingine yeyote.

²¹ Hakika sitaki kukosea, na afadhali niwe sahihi papa *hapa*, kwa sababu imechelewa sana nitakapofika *Huko*, mnaona. Unataka kuninii...Kama vile maskini yule ndugu mweusi asemavyo, “Sitaki shida yoyote mtoni.” Kwa hiyo, hiyo ni kweli. Ni—ninataka...Itakuwa asubuhi yenye ukungu, halafu wakati wa kutisha, nami hakika nataka tiketi yangu mkononi mwangu, imetiwa sahihi vizuri, maana si—sitaki...Imechelewa kupita kiasi wakati huo, mnaona.

²² Kwa hiyo, nami, katika kujadili jambo lolote ninaliendea nikajifunze jambo fulani, nataka kujua. Na kama nimekosea, bila shaka ninataka kujua kwamba nimekosea, unaona, ili niweze kuwa sahihi. Laiti ningalikubaliana na mambo hayo, na kuifanya kuwa ni hisia ya ulimwengu mzima, lakini mimi—mimi—mimi ninaninii tu, kama ni kosa, ni kosa tu. Ninyi... Hakuna ndege mweusi-mweupe wala mlevi-asiye mlevi, mnaona, a—ama ni kweli, au si kweli. Huwezi kuwa na kosa na kweli pamoja, ama ni kweli, au ni kosa. Mnaona? Mnaamini hilo, sivyo, ndugu? Na, bila shaka.

²³ Kama—kama Maandiko ni kweli, basi hebu na tudumu na Maandiko. Na kama kanisa ni kweli, basi, hivyo ndivyo nilivyowaambia hao makasisi, Nikasema, “Kama kanisa ni la kweli, dumuni na kanisa.”

Akasema, “Vema, kanisa ni la kweli.”

²⁴ Nikasema, “Basi, ulisema ya kwamba kanisa...kwamba ninii—kwamba Biblia, hapa, ni historia ya kanisa la kwanza. Vema, kama ndiyo, basi, kanisa lisiloweza kukosea, kwa nini mumebadilika sana?” mnaona. Basi hilo likatupa hoja yake huko nje, mnaona.

²⁵ Nikasema, “Ulisema Kristo aliunda kanisa Katoliki.” Mnaona? “Kama Yeye aliunda kanisa Katoliki, na kama mtume Petro na hao wote walikuwa ndio Wakatoliki wa kwanza, vema, basi mimi—mimi ni Mkatoliki, pia, basi, ninadumu na yale hasa waliyosema. Vema, ninyi mumeenda kombo sana hapa nje,” mnaona, nikasema, “huna lolote walilosema.” Mnaona? “Mbona, Petro alisema, yule papa wa kwanza, alisema, ‘Hakuna mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu, ila Kristo Yesu,’ Mpatanishi pekee, na sasa mna makumi ya maelfu yao.” Nikasema, “Sasa, yupi...? Je, yule papa wa kwanza ndiye sahihi, ama papa *huyu*? Ni yupi aliye sahihi?” Mnaona?

Akasema, “Vema, mnaona, kanisa Katoliki lina nguvu. Kato-...”

²⁶ Nikasema, “Yule Mkatoliki wa kwanza alisema lini basi, katika—katika kuliandika, kasema, ‘Kama Malaika kutoka Mbinguni akija akihubiri injili nyingine yoyote, na alaaniwe,’ awe ni papa, ama kasisi, ama yeyote yule, na,

‘yeyote atakayeondoa, au kuongeza katika Kitabu hiki, huyo ataondolewa...’” Nikasema, “Umechanganyikiwa kabisa mahali fulani, bwana. Ama kanisa lenu la kwanza liko sahihi, au *hili* liko sahihi. Na kama lenu la kwanza lilikuwa sahihi, *hili* haliko sahihi.” Mnaona? Nami nikasema, “Nitakaa na Wakatoliki wa kwanza.” Mnaona? Kwa njia hiyo walikuwa Wakatoliki. Kwa hiyo, mnaona, hamna budi kuwa sahihi.

²⁷ Tulininii tu... Kufanya ma—ma—majadiliano hamna budi kurudi kwenye jambo fulani, kimsingi, mnaloweza kuweka mikono yenu juu yake, kwa sababu una haki ya imani yako unayoamini, kadiri na kila mtu mwingine. Lakini hatuna budi kurudi, hapana budi pawe na mahali pa kuanzia, mahali fulani pa kusema, “*Hili* ndilo,” maana huwezi kubishana, kwa maneno mengine. Unaona?

²⁸ Kama sote wawili... Nikasema, “Vema, Maskani ya Branham iko sahihi,” nawe ungesema, yeye anasema, “Lile—lile—lile—lile,” mnasema, “Kanisa la Kianglikana liko sahihi, huko Uingereza, na—na...”

²⁹ Wasemaje? [Ndugu fulani anasema, “Vipi kuhusu Waarminia?”—Mh.] Naam, hebu na awe Muarminia, na kadhalika, mwajua, nawe chukua yale Matengenezo ya Uholanzi, vema sasa, tutaelekea wapi? Sasa, hapana budi pawe na mahali fulani. Vema, mnaweza kurudi nyuma na kunukuu katekismo zenu na zingine zote, na kadhalika. Tunataka kurudi kwenye kanisa, kwa waanzilishi we—wetu, mahali tulipoanzia, lakini tunaliwekea hili msingi wapi? Mnaona, hapana budi pawe na mahali ambapo hiyo ni kweli.

³⁰ Ni kama tu kanuni mnayozungumzia katika—katika Bunge, hamna budi kuwa na kitu kilicho sahihi. Huna budi—huna budi kuliweka huko nje na kuwaonyesha watu, na huna budi kuwa na mahali pa kuanzia. Vema, hivyo ndivyo inavyotubidi kuifanyia Biblia.

³¹ Kwa hiyo nikarudi kwenye—kwenye swali la Matendo 2 pamoja naye, Nikasema, “Sasa, u—unasema ya kwamba—ya kwamba Matendo 2 ndipo utakapo—utapoyawekea msingi.” Kwa hiyo, ilinibidi kumpa kitu cha kumwondosha—kumwondosha mstarini, kusudi aweze kuwa...aweze kuninii, niweze kuzungumza naye, mwajua, kumfanya atupiliwe mbali.

³² Nikasema, “Sasa, tuta—tutaninii, msingi—...kama wewe...” (Asante, ndugu.) “Kama utaninii tu, utadumu na Maandiko, sasa...” Nikasema, “Sasa, ndugu, na—navutiwa na msimamo wako.” Unaona? Nami nikasema, “Wewe ni... Ulisema hapa ya kwamba wote walijazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha zingine kama Roho alivyowajalia kunena. Walikuwako Yerusalemu, Wayahudi, watu watauwa kutoka kila taifa chini ya Mbingu, sauti hii iliposikika. Wakakusanyika pamoja, wakafadhaika, kwa sababu walimsikia

kila mtu akinena kwa lugha yake mwenyewe waliyozaliwa nayo.”

³³ Ilinibidi kumwongoza hapa kidogo, nikasema, “Sasa, ndugu, ningetaka kukuuliza hili: Sasa, kumbukeni, Biblia inasema ya kwamba hawa wasioamini, haikusema sasa, ya kwamba watu hawa, mnaona, hapa juu, walishuka kutoka kwenye mnara, kutoka juu kwenye chumba hiki cha juu jengoni, lilisema wote walijazwa na Roho Mtakatifu, na hawa hapa nje, walikuwa wakiwasikia katika lugha yao wenyewe waliyozaliwa nayo, mnaona. Waliwasikia, kila mtu. Mnaona? Wenye dhambi walikuwa wakiwasikia katika lugha yao waliyozaliwa nayo, wasioamini.” Kisha nikasema, “Basi kama fasiri yako ya Kipentekoste ni ya kweli, unaona, jinsi ulivyoliweka,” sasa, nikasema, “basi kuna kasoro fulani katika Matendo 2, ama kasoro katika fasiri yako.”

³⁴ Nikasema, “Sasa, ninataka kukuuliza, ndugu, ulimpokea wapi Roho Mtakatifu?” Akaniambia ile dakika, saa, na wakati, mtu mwema, mnaona. Naye, kidogo mwenye kiburi, mwajua, kidogo amekasirika, kwa kuwa alitokwa jasho. Hakuna sababu ya hilo. Mnaona?

³⁵ Kama nina sungura aliyefungiwa kondeni, wala kamwe hana njia ya kutokea, nitasimama langoni, hana budi kurudi, maana hatoki. Kwa hiyo si lazima ulitolee jasho, kama unaweza kujua hasa, unajua hakuna shimo popote kwa ajili yake kutokea. Kwa hiyo unaweza kudumu moja kwa moja katika Andiko lolote unalotaka, hana budi kurudi kwa hilo. Mnaona? Kwa hiyo, ha—haendi popote, haikubidi kumfukuza kote uwanjani, simama tu hapo na umwache akurudie.

³⁶ Kwa hiyo basi nikasema, “Bwana,” nikasema, “sasa, ulitendaje ulipompokea Roho Mtakatifu?”

Akasema, “Mungu asifiwe! Nilinena kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.”

Nikasema, “Vema, ni akina nani wote waliokuwa pale?”

Kasema, “Karibu watu mia moja na hamsini.”

“Mlikuwa kanisani?”

“Naam, bwana.”

“Na wote walikuwa watu wanaozungumza Kiingereza?”

“Naam.”

Nikasema, “Basi ulinenaje?”

Naye akasema, “Nilinena kwa lugha.”

Nikasema, “Katika kunena kwako, ulitoa ushuhuda wa Roho Mtakatifu?”

“Naam, naam.”

“Kwamba ulikuwa umempokea Roho Mtakatifu?”

“Naam.”

“Je, kusanyiko lilikuelewa?” Mnaona?

Akasema, “Kwa nini, la.”

³⁷ Nikasema, “Basi haikuwa ni kulingana na Matendo 2:4, basi, unaona,” Nikasema, “kwa sababu kila mtu alisikia katika lugha yake mwenyewe aliyozaliwa nayo. Hakuna maneno yaliyofichika hata kidogo, kila mtu alisikia katika lugha yake mwenyewe aliyozaliwa nayo.” Nikasema, “Basi hakika hukupata kulingana na Matendo 2:4.” Hilo likaondoa Andiko hilo papo hapo kutoka kwake, wasimamizi wakanipa ushindi, mnaona, papo hapo, mwajua.

³⁸ Nikasema, “Sasa, kwenye Siku ya Pentekoste wao, kila mmoja, alisikia katika lugha yake mwenyewe, hayakufichwa hata kidogo.”

³⁹ Akasema, “Loo, naona mahali ulipochanganyikiwa, Ndugu Branham.” Akasema, “Unaona, Ro—Roho Mtakatifu, wakati alipokuja mara ya kwanza,” alisema, “kuna...tunanena kwa lugha ya Malaika, unaona,” akasema, “hakuna—hakuna tafsiri yake. Lakini basi unapopata tafsiri,” akasema, “halafu kuna lugha zinazoweza kufasiriwa katika baadhi yao, kama Paulo alivyosema.”

⁴⁰ Nikasema, “Naam, bwana, ninaelewa hilo.” Nikasema, “Basi unataka kuniambia basi, bwana, ya kwamba—ya kwamba tunapompokea Roho Mtakatifu, hiyo ndiyo lugha ambayo hakuna mtu anayeielewa,” mnaona, “tunaponena kwa lugha, hapo tunapompokea Roho Mtakatifu?”

Akasema, “Jambo ndilo hilo.”

⁴¹ “Halafu baada ya kubatizwa na kuingia katika ule Mwili, ndipo tunapokea lugha ambazo—ambazo zinaweza kufasiriwa, unaona. Ndivyo hivyo?”

“Naam.”

⁴² Nikasema, “Basi umepindua mambo.” Mnaona? Nikasema, “Basi inakubidi, hapa,” unaona, nikasema, “basi kwenye Siku ya Pentekoste walipompokea Roho Mtakatifu walimpokea tofauti na ninyi nyote.” Nikasema, “Nyote mnampokea na hakuna mtu anayeielewa, walipompokea kila mtu alielewa,” Nikasema, “ama, jamaa hawa walikuwa na karama huko nje ya kufasiri.” Mnaona?

⁴³ Kisha nikasema, “Basi ukiwapa karama ya kufasiri, basi wao walikuwa na Roho Mtakatifu, pia, maana walikuwa na tafsiri, kadiri ulivyo na karama ya kunena, huku walikuwa wakiwatania, wakiwadhihaki.” Mnaona? Mnaona, halina msingi wowote. Na kwa hiyo, basi nikasema, “Vipi kama nilikwambia ya kwamba Mungu aliwafanyia watu hawa jambo fulani hata wao...hawa...kila mtu, sasa, aliwasikia katika lugha yao wenyewe?”

Akasema, “Lakini walikuwa wakinena kwa lugha.”

44 Nikasema, “Hebu kidogo, ndugu, asiyeamini huko nje alisema, ‘Tazama, si hawa wote wanaonena ni Wagalilaya, nasi twawasikiaje kila mtu katika lugha yetu tuliyojaliwa nayo? Hawa wanenao ni Wagalilaya, wakinena Kigalilaya, bali tunayasikia katika lugha yetu wenyewe tuliyojaliwa nayo.’” Mnaona, asingeweza kusimama popote basi, mnaona. Mnaona? Nikasema, “Sasa...” Akasema... Nami nikasema, “Mimi...” Hiyo ingeweza kuwa hivyo,” nikasema, “nimeona hilo likitukia.”

45 Maskini msichana Mhispania wakati mmoja, nilikuwa nikiwaambia habari zake, nadhani mumeisikia kwenye kanda, mwajua. Na kwa hiyo, nikasema, “Sasa, sisi... Nilikuwa nikizungumza tu kama ninavyozungumza sasa, naye alikuwa akinisikia, na papo hapo, ndipo akamwambia mkalimani, ‘Nilifikiri asingeweza kuzungumza Kihispania.’ Vema, tukacheza hiyo kanda tena na ilikuwa ni Kiingereza, lakini wakati uvuvio ulipokuwa ukiendelea, alisikia katika Kihispania, halafu basi asingeweza kusikia moja, ama, hakuelewa hata neno moja katika Kiingereza.” Mnaona?

46 Kwa hiyo, ilikuwa ni kwa ajili yake, kamwambia yote aliyokuwa nayo, kifafa, naye ameketi karibu na mekoni akila mahindi ya manjano, akala kupita kiasi ndipo akawa mgonjwa sana, akaenda kitandani, na kushikwa na kifafa, alikuwa nacho tangu wakati huo, mnaona, mpaka wakati huo, akaponywa.

Kwa hiyo akasema, “Vema, sasa hebu kidogo.” Akasema, “Walikuwa... Ninaona ambapo wewe...”

47 Kisha nikasema, “Nashangaa tu, ndugu, ni kwa nini, wakati ulipopewa swali hili,” nikasema, “ulikuwa ukizungumza juu ya Matendo 2:4, kisha ukaenda kwenye Matendo 10:49,” Nikasema, “uliachaje Matendo 8, wakati Wasamaria walipompokea Roho Mtakatifu? Hakuna Maandiko yanayosema ya kwamba walinena kwa lugha.” Unaona?

48 Vema, nikasema—nikasema, “Kama ukiangalia huko Yerusalemu, kulikuwa kumekusanyika, ninauchukua upande wako sasa, unaona,” nikasema, “kulikuwa na watu wamekusanyika kutoka mataifa yote,” anaendelea na kuwataja, Wamed na Waajemi, na—na waongofu, na wageni, na Wamakedonia, loo, mwajua, wote namna hiyo, mahali walipokuwa, nikasema, “sasa, wote walikuwa—wote walikuwa pale, nao waliwasikia, kila mtu katika lugha yake mwenyewe.

49 Nami nikasema, “Sasa, na katika nyumba ya Kornelio,” sasa, nikasema, “wakati waliponena kwa lugha pale, walisikia katika lugha yao wenyewe, jambo lile lile walilofanya *huku* nyuma,” nikasema, “kwa sababu kwamba Petro alisema, ‘Tunaweza kuzuia maji, kwa kuwa hawa wanapokea Roho Mtakatifu kama sisi hapo mwanzo?’” Nikasema, “Mungu kamwe hatabadilisha mpango Wake; kama utasimama papa hapa kwenye Matendo 2,

papa hapa ambapo Roho Mtakatifu alishuka mara ya kwanza, lita—litashirikiana na hayo mengine.”

⁵⁰ Nikasema, “Sasa, kama ni muhimu hivyo, kwa nini Wasamaria hawakunena kwa lugha walipompokea Roho Mtakatifu?” Nikasema, “Kwa sababu wote waliongea Kiyahudi. Mnaona? Mnaona, wote waliongea Kiyahudi. Hakukuwa na haja ya wao kutumia lugha nyingine, kwa sababu walishuhudia tu kwamba Roho Mtakatifu alikuwa amekuja, wote walikuwa wakiongea kwa lugha yao, na—na, kila mtu,” ba—basi nikasema, “wala hapakuwa na sababu yake.”

⁵¹ Nikasema, “Hayo hapo yale makabila matatu, unaona, Wayahudi, Wasamaria, na Mataifa.” Tena nikasema, “Sasa, Mataifa, kama unakumbuka, Kornelio alikuwa akida juu ya watu mia moja, kikosi cha Waitalia. Kulikuwako na waliotahiriwa na Warumi, na Waitaliano, na—na wote—wote pamoja kule, na vyovyote ilivyokuwa, alikuwa akinena, ‘Kwa sababu, kama tu ilivyokuwa hapo mwanzo, sasa, je, tunaweza kuzuia maji kwa kuwa hawa wamempokea Roho Mtakatifu kama tulivyompokea hapo mwanzo?’ Kwa hiyo, mnaona, ilibidi iwe vile vile ilivyokuwa hapo mwanzo, na kila mtu ilimbidi kusikia kwa lugha yake mwenyewe.”

⁵² Nikasema, “Nitakubali kwamba kulikuwako na wakati mmoja, ambapo, katika Biblia, ambapo kila mtu alinena kwa lugha.”

Bila shaka, alikuwa amefadhaika sana, mwajua, naye akasema, “Haleluya! Sasa, uko njiani!”

⁵³ Nikasema, “Naam, bwana, hiyo ilikuwa huko Babeli, hakuna mtu aliyelewa yale huyo mwingine aliyosema.” Nikasema—nikasema—nikasema, “Kwenye Pentekoste, wote walielewa yale kila mtu aliyosema,” Nikasema, “ilikuwa ni kule kutoka kwa Roho Mtakatifu, mnaona.” Nikasema, “Huko Babeli, wote walinena kwa lugha zisizojulikana, kama vile Pentekoste ifanyavyo sasa. Hakuna anayejua yale mwingine anasema, mmoja akipayuka—payuka *haya*, mmoja akipayuka—payuka *yale*, wala hawakujua kitu, bali hiyo ilikuwa Babeli, mnaona, lakini,” nikasema, “huko Pentekoste kila mtu alisikia katika lugha yake mwenyewe, ambayo alizaliwa nayo.”

Naye akasema, “Vema, mimi—mimi . . . Wewe ni—wewe ni . . . ningali ninaamini.” Kasema, “Utukufu kwa Mungu, ninaupokea. Haleluya! Unalifanya Kanisa kuwa na nguvu zaidi.”

⁵⁴ Nikasema, “Sasa ngoja, hatuzungumzii hilo, tunazungumza juu ya Fundisho la Biblia, unaona. Tunadumu na Maandiko hapa, unaona.”

⁵⁵ Na—na kwa hiyo basi tulipokuwa tukiendelea, alisema, “Vema,” akasema, “loo, ninaamini wote walikuwa chini ya uvuvio, wakinena kwa lugha.” Akasema, “Siamini waliyasikia kutoka kwa fasiri, ninaamini walivuviwa, wakinena kwa lugha.”

⁵⁶ Nikasema, “Nitakubaliana nawe kwa hilo, nasi tutamaliza mjadala wetu juu ya jambo hilo,” mnaona, “kwamba wote walivuviwa, wakinena kwa lugha.” Kisha nikasema, “Sasa unaona, ni kama tu,” nikasema, “sote tumekusanyika hapa Jeffersonville,” sote tumekusanyika hapa Yakima, “Sikukuu ya Pentekoste inaendelea.” Ndipo nikasema, “Sasa, tutasema kwamba wewe *ni* Mswisi, wewe *ni* Mjerumani, nawe *ni* Mfaransa.” Mnaona? “Nasi sote tuko hapa ndani, na kila mmoja wenu ni kundi la watu.

⁵⁷ “Sasa, tuseme ni mimi mwenyewe, na Ndugu Borders, na Ndugu Gene aliyeketi hapa, nasi sote ni Wamarekani. Mnaona? Na *wewe* una kundi, *wewe* una kundi, *wewe* una kundi, maana hivyo ndivyo walivyokuwa, walikuwa Wamedi, na Waajemi, na kadhalika wamekusanyika kule.”

⁵⁸ Ndipo nikasema, “Sasa, sisi—sisi sote tuko hapa, na kwa ghafla inakuja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, unaijaza nyumba humu ndani, si huko nje pamoja nanyi nyote, nami nilikuwa *hapa*. Sote tukajazwa na Roho Mtakatifu, nasi tukatoka nje, na muda si muda mwajua hapa, mimi—mimi ni Mwingereza, nami ninaanza kuzungumza katika Kiingereza,” jinsi nilivyokuwa kwanza, mnaona, “nanyi mnayaelewa katika Kiswisi.”

“Loo, la. La, la.” Akasema, “La, ulikuwa ukizungumza katika—katika—katika,” samahani, “katika Kiulaya.”

⁵⁹ Nikasema, “Basi kama ndivyo ilivyokuwa, basi ninamwambia nini? Kuhusu kufufuka kwake Yesu Kristo, juu ya kuja kwa Roho Mtakatifu.” Mnaona? Nikasema, “Ni—ninaongea na *wewe* Mswisi, wakati Gene akizungumza na *nyinyi* katika Kijerumani, na Roy anazungumza na *nyinyi* katika Kifaransa.” Mnaona? Naye akasema... Nikasema, “Basi...”

Akasema, “Sasa—sasa, u—uko karibu sana nalo.”

⁶⁰ Nikasema, “Ati karibu sana nalo?” Nikasema, “Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema, ‘Tunasikia kila mtu katika lugha yetu, tuliyojaliwa nayo.’” Mnaona?

⁶¹ Akasema, “Loo.” Nao wasimamizi... Tayari nimeliona, tayari nimewekewa alama ubaoni kila moja umbali huu, mwajua. Kwa hiyo nikasema, “Tutamaliza hili.” Naye a—akasema... Na—nami nikasema, “Basi wote walikuwa—wote walikuwa wakizungumza, wakielewana.” Ambalo tayari nilikuwa na hilo kwenye, lililokamatwa kwa kuanzia. Iliwabidi kuelewa lugha yao, mnaona, Babeli ulikuwa ndio wakati pekee ambao hawakuelewa, Pentekoste, walielewa, kila mtu.

⁶² Hiyo, Injili haina budi kwenda ulimwenguni kote, kuanzia Yerusalemu, nayo ilienea kote ulimwenguni wakati huo, ulimwengu unaojulikana, papo hapo. Mnaona? Ilibidi ije namna hiyo, maana, mnaona, mataifa yote chini ya Mbingu

yalikusanyika pale, mataifa ya kidini, ilikuwa ni Pentekoste. Mnaona? Naye akaufikia ulimwengu mzima, “Lakini enendeni ulimwenguni kote,” kuanzia Yerusalemu. Mnaona? Kwa hiyo ilibidi ishuhudiwe katika lugha ya kufufuka kwake Kristo, ipate kuenea ulimwenguni kote papo hapo. Mnaona? Na hawa wabebaji hapa, watu hawa hapa ndani, waabuduo, wangerudi nchini mwao.

⁶³ Kama vile siku chache baada ya hapo yule Mkushi akishuka, mwajua, naye Filipo alikuwa huko chini Samaria, naye Mkushi alikuwa njiani akirudi Afrika, yule towashi, ndipo Roho Mtakatifu akamwita Filipo kutoka kwenye mkutano huo mkubwa, akamfanya asimame jangwani. Alikuwa akisoma Isaya. Akasema, “Unasoma nini?”

⁶⁴ Akasema, “Ninawezaje kujua isipokuwa mtu fulani anifundishe?” Alikuwa akisoma, kasema, “Ni nani—ni Nani ambaye nabii alikuwa akinena habari zake, yeye mwenyewe au...?” Alikuwa huko juu kwenye Pentekoste kuabudu. Mnaona?

⁶⁵ Kwa hiyo akambatiza papo hapo katika Jina la Yesu, naye akaenda zaje Ethiopia akishangilia, akiupeleka Ujumbe Ethiopia. Huko ndiko ulikopaswa kuwa, uende. Sasa, hii hapa inakuja ninii... Hili—hili hapa. Mnaona?

⁶⁶ Nikasema, “Sasa...” Kwa hiyo, nikasema, “Unaona, bwana, kwamba hata wasimamizi tayari wameweka alama huko juu, kwamba wao—wao walinena katika lugha ambazo kila mtu alielewa, hakuna hata neno moja lililoachwa.” Mnaona? “Kwa hiyo toleo lenu la Pentekoste tayari limehukumiwa, mnaona, kwa sababu, itakubidi kuweka toleo lako la Pentekoste huko Babeli, maana huwezi kuliweka katika Matendo 2:4.” Mnaona? “Kwa kuwa walisikia kila mtu katika lugha yake mwenyewe aliyozaliwa nayo, wala huko Babeli hapana mtu aliyefahamu chochote. Kwa hiyo, unaona, toleo lako la Kipentekoste tayari limerudi katika Mwanzo tena, huko Babeli, unaona, kwa hiyo wewe huko juu hapa Pentekoste, tena.”

⁶⁷ Nami nikasema, “Lakini hebu na tuunde mbele kidogo,” mnaona, “kwa sababu tayari tumepewa, mnaona, pale. Kwa hiyo kila mahali uendapo katika Biblia, halina budi kurudi kama lilivyofanya hapo mwanzo, Mungu hana kikomo wala hawezi kubadilika.”

⁶⁸ Akasema, “Vema, wao...” Ndipo akaanza kwa hayo mengine, akasema, “Sasa, utakubali, hata hivyo, Ndugu Branham, ya kwamba watu hawa waliotoka *hapa* hawakuwa tu kama Wamethodisti au Wabaptisti.” Mnaona, hilo, akiwashambulia Wabaptisti wangu, mnaona. Kasema, “Hawakuwa... Walikuwa wamepokea na walikuwa wakinena chini ya uvuvio.”

69 Nikasema, “Naam, bwana, nitakubaliana na hilo.” Kwa hiyo wakalitia hilo alama. “Nitakubali ya kwamba wa—walikuwa wakinena chini ya uvuvio, yale waliyokuwa wakisema.” Nikasema, “Kila wakati ninapohubiri, ninahubiri vivyo hivyo, nawe je? Chini ya Kiingereza, wajua, kwa uvuvio.” Hivyo—hivyo tu ndivyo walivyo kabisa, mwajua...?... Nikasema, “Kila wakati ninapohubiri au kutabiri, si katika lugha zisizojulikana. Paulo alisema kama haikuwa na mfasiri kwamba haikuwa kitu, kama mjinga, Haina budi kuwa ni ya kujenga, na kadhalika, mnaona.” Kwa hiyo hilo lilimtolea hilo. Mnaona?

70 Nikasema... Vema, akasema... Nami nikasema, “Vema, ninakubali kwamba yote yalikuwa chini ya uvuvio.” Nikasema, “Sasa—sasa, namna hii,” nikasema, “baadhi yao sasa,” nikasema, “kama tulivyokuwa...” Nikasema, “Wale basi waliokuwa wakizungumza na Wagalilaya huko Galilaya, walikuwa chini ya uvuvio, sivyo?” Mnaona? “Kama vile kama sisi sote ni Waingereza...”

Akasema, “Hakuna hata mmoja wao Mgalil-...”

71 Nikasema, “Ilikuwa huko Galilaya, nao wote waliokuwa wakinena walikuwa Wagalilaya, kulikuwako na Wagalilaya huko wakiwasikia, kwa sababu walikuwa Galilaya, hiyo ilikuwa katika lugha ya taifa.” Nikasema, “Ndipo mtu *huyu* akaja, naye akaongea na Wagalilaya katika lugha yao ya kienyeji, naye alikuwa Mgalilaya, kama vile tu mimi ni Mwingereza, nikizungumza na Mwingereza, katika Kiingereza.” Mnaona? Naye hakuwa nayo, mnaona.

Vema, akasema, “Huenda ilimwangukia mmoja, halafu huyo mwingine, waliigawanya tu. Labda huyu *hapa* angekuja azungumze nao kwa muda kidogo.”

72 Nikasema, “Ndipo baada ya maskini hao Wagalilaya, basi hawakusikia chochote.” Nikasema, “Hakuwa amevuviwa basi wakati alipokuwa akizungumza nao juu ya ufufuo. Jambo lile lile.” Mnaona, hakuna mahali pengine pa kusimama, tena.

73 Nasi tuliendelea tu namna hiyo mpaka tukayachunguza Maandiko kwa makini sana, tukaendelea moja kwa moja hivyo. Mnaona? Itabidi irudi kwenye ile ya asili, ya kwanza. Unaona?

74 Kwa hiyo mnaona, ni...Pale...Si kunena kwa lugha isiyojulikana, ni kunena chini ya uvuvio. Mnaona? Na kama vile, kama nikimpokea Roho Mtakatifu hapa asubuhi ya leo, katikati yenu nyote, ningekuwa chini ya uvuvio nikiwaambia juu ya ufufuo wa Roho Mtakatifu ulionijia, chini ya uvuvio. Sasa, mnaona, lugha si Roho Mtakatifu. Mnaona?

Ndipo akasema, “Basi huamini katika kunena kwa lugha?”

75 Nikasema, “Bila shaka, ninaamini. Ninaamini katika kunena kwa lugha.” Kisha nikasema, “Ndiyo iliyo ndogo sana miongoni mwa karama—karama, kulingana na vile

ilivyoandikwa katika Biblia, maana ndiyo karama ya mwisho.” Mnaona? Nikasema, “Basi mtu angenena kwa lugha, lakini kwanza hana budi kuwa na Roho Mtakatifu kabla yeye—yeye hajanena kwa lugha, kama sivyo, yeye ni mwigaji.”

⁷⁶ Nikasema, “Basi angeweza kunena kwa—kwa lugha, kama ulivyosema, za wanadamu na za Malaika pia, na bado asiwe na Roho Mtakatifu,” nikasema, “kwa sababu Paulo alisema, ‘Nijaposema,’” japo ninaweza, “kunena kwa lugha za wanadamu na za malaika wala sina upendo, si kitu mimi. Nijapoweza kuelewa maarifa yote, na ninaweza kufasiri Maandiko vizuri kabisa, bila ubatizo huu, si kitu mimi. Na nitoe mali yangu kuwalisha maskini, na mwili wangu uhomwe moto kama dhabihu, na imani ya kuhamisha milima, si kitu mimi, hata sijaanza bado, mnaona, nami nina imani hii yote.”

⁷⁷ Nikasema, “Sasa, hilo linajibu kama Dk. Hegre kule juu wakati ule,” mwajua, yule mshauri Mlutheri, mwajua nilipomwambia, mnakumbuka ule mjadala tuliokuwa nao, mwajua, pale juu ya, juu ya, kuhusu, alikuwa akiniambia kuhusu yule mwanamke mchawi, mwajua, aliyewaombea wagonjwa, waliponywa, kasema Mungu asingeweza kuponya. Mmesikia hilo. Mnaona? Mnakumbuka hilo? Mnaona?

⁷⁸ Nikasema, “Vema, tuna wengi wa watu hawa waliojitokeza, kasema, ‘Ndugu, nina uponyaji mkononi mwangu. *Whiu!* Ati kuuhisi?’ Hawauhisi, bali watu wanaponywa vivyo hivyo, maana ni juu ya msingi wa imani, naye huyo jamaa anafikiri anamkaribia Mungu hivyo. Nami ninaamini wengi wa watu hawa wanampokea Roho Mtakatifu,” mnaona, “walipotoka huko wakinena kwa lugha. Hakika, ninaamini ni Roho Mtakatifu, lakini huo sio ushahidi kwamba wanaye, maisha yao yatakuwa na matunda. Baadhi yao walitoka huko na—na...”

⁷⁹ Mlisikia ono langu, nadhani mmesikia kwenye kanda zangu jinsi ambavyo wakati nilipoenda Mishawaka wakati ule, hao watu, wakija kule, mwajua, wakati yule mvulana mweusi aliposema, “Huyu hapa! Huyu hapa!” mnajua? Vema, mnakumbuka, walikuwa na mtu mmoja pale akinena kwa lugha na huyo mwingine akifasiri. Sikuwahi kuisikia hapo kabla maishani mwangu. Mnaona? Na sasa, kama ningewaambia, mngenicomesha. Mnaona?

⁸⁰ Kwa hiyo basi, lakini jamaa huyu alishindwa huo mjadala, mwajua. Bila shaka kuna mengi zaidi, lakini mnaona kile ninachozungumzia hapo. Mnaona? Rudini moja kwa moja mwanzoni, mnaona, rudini moja kwa moja kwenye mwanzo.

⁸¹ [Ndugu fulani anasema, “Kuna wengi wa watu hawa wanaonena kwa lugha, na kujisikia wana huo ubatizo, lakini wao—wao kwa kweli hawana.”—Mh.] Hawana. [“Wamekiri,”—Mh.] Naam. [“kuwa nao, bali wao...”] Hawana, mnaona. Wakati Roho Mtakatifu wa kweli anapoingia, ni Uhai wa Kristo,

mnaona, unaoishi katika mwanadamu, mwanadamu. Mnaona? Wala hawakusema neno juu ya Yesu kunena kwa lugha wakati alipompokea Roho Mtakatifu.

⁸² Sasa, vipi kuhusu Yohana Mbatizaji? Alimpokea Roho Mtakatifu miezi sita kabla hajazaliwa, katika tumbo la uzazi la mama yake. Alinenaje kwa lugha?

[Ndugu fulani anasema, “Vipi kuhusu kiziwi na bubu?”—Mh.]

⁸³ Naam. Wangewezeje kunena kwa lugha, kama hata wasingeweza kuongea wala kusikia? Mnaona?

⁸⁴ Vipi kuhusu Elisabeti na Mariamu wakati wao . . . “Elisabeti, mamaye Yohana, alipojazwa na Roho Mtakatifu, na kutabiri, akisema,” si akinena kwa lugha. Mnaona?

⁸⁵ Kwa hiyo wao—wasingeweza kujitetea . . . Nilizungumza na baadhi ya viongozi wao wakuu hata hivyo, na watu wa halmashauri kuu wenye akili wata—watakubali hilo, mnaona, lakini wao . . . Lakini walisema nini? “Yote, hayo ni fundisho la Kanisa,” mnaona. Hilo ndilo . . . Mtafanya nini juu yake? Vema, haya basi. Mnaona? Sasa, kile . . . Kama walijaribu kubadilisha hilo sasa, wangewafukuza kutoka madhehebuni. Mnaona? Vema, hiyo hasa ni . . .

⁸⁶ Ninaweza kukaa huru, si lazima niwe na dhehebu lolote. Mnaona? Mimi ni raia aliyezaliwa huru, na nina haki ya kuzungumza, na—na lolote ninalotaka kusema, uhuru wa kuongea. Nami ni mhudumu aliyewekwa wakfu, na kwa hiyo hawawezi kunizuia kufungisha ndoa, kuzika, ama kubatiza, ama kuhubiri Injili, mnaona. Maadamu sisi ni demokrasia, si lazima tuwe wafuasi wa shirika lolote, mnaona. Na—na kwa hiyo sasa, tu—tu—tunasema hili kama . . . kwa kuwa—kwa kuwa . . . Mnaelewa sasa? Mmeshawishika kabisa? Naam, kwamba ni . . . nisingeninii . . . Mnafikiri kuna mambo ambayo huenda—huenda yakaonekana ni mazuri sana, sana . . . ? . . . kwamba Maandiko hayana budi kuafikiana kikamilifu. 

60-0807 Mjadala Juu Ya Lugha
Unknown
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org